# HOJA BATILI DHIDI YA DA'AWA YA KWELI

Mwandishi:

ABU HASHIM ABDUL - QADIR

ALLAH AMHIFADHI

# HOJA BATILI DHIDI YA DA'AWA YA KWELI

# UTANGULIZI

Sifa njema zinamstahiki Allah subhanahu wa Taala na swala na salam zimshukie mtume wetu Muhammad na jamaa zake na maswahaba wake wote.

Asili ya kijitabu hiki ni muhadhara nilioufanya Masjid Aishah hapa Mombasa mwezi wa kwanza (Muharram) 1430, katika jumla ya Mihadhara ya kila jumamosi ya mwisho wa kila mwezi inayofanywa na walinganizi (Duat) wa daawa Salafiyya hapa Mombasa.

Baada ya muhadhara huo, ndugu yetu Abu Bakr Khatwiyb anayeishi Sweden aliutoa muhadhara katika CD na kusaidia kijitabu hiki ili wapate kufaidika wengi ambao hawakuhudhuria hapo Masjid Aishah. Pia ndugu yetu Abu Bakr Kwatwiyb - Allah amuhifadhi- alifanya juhudi nyingine kubwa kwa kubainisha zaidi chini ya kijitabu hiki na kuchomekea baadhi ya sehemu kwa kueleza mifano hai.

Maadui wa Daawa hii ya haki wanatoa shubha (hoja batili) nyingi ili kuichafua daawa salafiyya ambayo ndiyo daawa pekee iliyo na dalili katika Quraan na sunnah. Maulamaa waliotangulia na hawa wa sasa wamezirudi na kuzichangua shubha hizo kwa mapana na marefu.
Allah awajaze kila la kheri wote waliosaidia katika kukifanikisha kijitabu hiki kwa njia moja au nyingne.

Natarajia kuwa pindi tu utakapokimaliza kukisoma kijitabu hiki utapata faida nyingi na wewe mwenyewe utaweza kuzibatilisha shubha hizo za mahizbi na wengineo.

# 02. HII NDIO DA'WAH YETU

Ndugu waislamu! Mfumo na mwongozo wetu ni kufuata Qur-aan, Sunnah kwa ufahamu wa as-Salafu as-Swaalih[1]. Huu ndio mfumo wetu. Huu ndio mfumo wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa ah na khaswa Salafiyyuun. Huu ndio mfumo, mwongozo, nidhamu na sera yao. Wao wanafuata Qur-aan, Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kwa ufahamu wa wema waliotangulia ambao ni Maswahabah, Taabi'uun na waliokuja baada ya Taabi'uun.

Ndugu waislamu! Nimeanzia kusema hivyo kutokana na kwamba kuna watu wanaojiita kuwa wao ni Ahl-us-Sunnah kumbe sio. Kuna watu wanajiita na kujigamba kuwa wao ni Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah, lakini ukweli ni kwamba wao sio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah wa sawasawa ni hawa wanaofuata Qur-aan na Sunnah kwa ufahamu wa watu wema waliotangulia. Hawa ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa ah. Vilevile hawa ndio kundi lililookoka, kundi lililonusuriwa na kundi kubwa[2]. Ahl-us-Sunnan wal-Jamaa'ah ndio Salafiyyuun.[3]

---

**1.** Wema waliotangulia. Makusudio ni Maswahabah, Taabiuun na waliokuja baada ya Taabi'uun. Hili ni kutokana na kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amezisifia karne hizi tatu na kwamba ndio karne bora pindi aliposema:

"Wabora wenu ni karne yangu. Kisha watakaofuatia. Kisha watakaofuatia." Mpokezi anasema: "Sikumbuki baada ya karne yake alitaja karne mbili au tatu." al Bukhaariy (6690), (6428), (365) na (2651) na Muslim (2525) na (214)

**2.** As-Sawaad al-A'dhwam. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema: "**Ummah huu hauwezi kukusanyika katika upotevu. Mkono wa Allaah uko juu ya al Jamaa ah. Kwa hivyo shikamaneni na kundi kubwa na yule mwenye kuukhalifu, basi amekhalifu kwenye Moto.**" (Ibn Abiy Aaswim (80) na al-Haakim (1/115-117)).

Imaam Ibn-ul Athiye al Jazariy (Rahimahu Allaah) amefasiri neno "as Sawaad al-A'dhwam" na kusema: "Kundi kubwa la watu ni wale waliokusanyika katika kumtii mtawala na kushikamana na mfumo uliyonyooka." (an Nihaayah (1/822).

**3.** Firqat-un-Naaniyah na Twaaifat-ul-Mansuurah. Wana majina mengi zaidi ya hayo aliyotaja Shaykh (Hafidhwan Allaah) ambayo yote yanarejea katika neno hilo hilo moja. Miongoni mwa majina yao vilevile ni Ahl-ul-Hadiyth, Ahl-ul-Athar na mengineyo.

Allaamah Swaalih bin Fawzaan al-Fawzaan (Allah Amhifadhi) amesema alipokuwa akieleza maana yao makuu na yanayotumika sana: Firqat-un- Naajiyah, Twaaifat-ul-Mansuurah na Ahl us Sunnah wal-Jamaa'ah, yafuatayo:

Ilipokuwa kundi hili ndilo lililosalimika kutokamana na upotevu, jambo linapelekea kujua majina na alama zake ili mtu aweze kulifuata. Lina majina matukufu yanayolipambanua na mapote mengine.

Huu ndio mfumo wetu; ni kufuata Qur-aan na Sunnah kwa ufahamu wa wema waliotangulia. Jambo hili ni wajibu kwa kila muislamu. Kila muislamu anawajibika kufuata mwongozo na mfumo huu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake. Dalili katika jambo hili ni nyingi katika Qur-aan.

Katika Suurah "at-Tawbah" Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amesema:

﴿وَٱلسَّٰبِقُونَ ٱلۡأَوَّلُونَ مِنَ ٱلۡمُهَٰجِرِينَ وَٱلۡأَنصَارِ وَٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُم بِإِحۡسَٰنٖ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُ وَأَعَدَّ لَهُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي تَحۡتَهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدٗاۚ ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ﴾

---

= Miongoni mwa majina na alama muhimu zaidi ni: kundi lililookoka, pote lililonusuriwa na Ahlu Sunnah wal-Jamaa'ah. Maana yake ni kama zifuatazo:

**Ya kwanza:** Kundi lililookoka ina maana kwamba ni kundi lililookoka kutokamana na Moto pindi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipolivua wakati alipokuwa anataja kuhusu mapote na akasema: "Yote yataingia Motoni isipokuwa moja tu."
Bi maana [hili moja] ndilo halitokuwa Motoni.

**Ya pili:** Ni lenye kushikamana na Qur-aan na Sunnah za Mtume wake na yale waliyokuwemo wa awali waliotangulia katika Muhaajiruun na Answaar pindi aliposema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuwahusu:
**"Ni wale wataofuata yale ninayofuata mimi hii leo na Maswahabah wangu."**

**Ya tatu:** Watu wenye kundi hilo ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa 'ah. Wamejipambanua kwa sifa mbili kuu:

**1-** Wameshikamana na Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) mpaka watu wake wakawa hivo tofauti na mapote mengine ambapo wameshikamana na maoni, matamanio na maneno ya viongozi mfano wa hao. Hayajinasibishi na Sunnah. Yamejinasibisha na Bid'ah na upotevu wake – mfano wa hao ni Qadariyyah na Murji ah - au kwa maimamu wao mfano wa hao ni Jahmiyyah au kwa matendo yao machafu - mfano wa hao ni Raafidhwah na Khawaarij.

**2-** Watu wa al Jamaa'ah. Hili ni kwa sababu ya kukusanyika kwao juu ya haki na kutofarikiana. Hili ni tofauti na mapote mengine. Wao hawakusanyiki juu ya haki. Bali wanakusanyika juu ya matamanio yao. Hakuna haki inayowakusanya.

**3-** Ni kundi lililonusuriwa mpaka siku ya Qiyaamah kwa sababu limeinusuru dini ya Allaah na hivyo Allaah na Yeye akawa amelinusuru. Amesema (Ta'ala);

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِن تَنصُرُواْ ٱللَّهَ يَنصُرۡكُمۡ وَيُثَبِّتۡ أَقۡدَامَكُمۡ﴾

**" Enyi Mlioamini, Mkimnusuru Allaah Naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu." (47:07)**

Kwa ajili hii Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema juu yake:
"**Halitodhurika na wale wenye kuwakosesha nusura wala wenye kwenda kinyume nao mpaka kifike Qiyaamah lihali wako katika hali hiyo**" al-Bukhaariy (3442), Muslim (1037) na Ahmad (04/93)"

**"Na wale waliotangulia wa mwanzo miongoni mwa Muhaajiruun na Answaar na wale waliowafuata kwa wema, Allaah ameridhika nao, nao wameridhika Naye. Na Amewaandalia mabustani ipitayo chini yake mito ni wenye kudumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa" (09:100)**

Hii ni moja katika Aayah na dalili ambazo kila muislamu anawajibika kufuata mwongozo huu. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amewasifu Maswahabah ambao ni Muhaajiruun na Answaar na kila atakayewafuata wao kwa wema. Kila ambaye atawafuata Muhaajiruun na Answaar kwa wema, basi Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amemsifu katika Aayah hii na kumuahidi kuwa atamtia Peponi:

﴿وَٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُم بِإِحْسَٰنٍ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُواْ عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّٰتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًاۚ ذَٰلِكَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ﴾

**"...na wale waliowafuata kwa wema, Allaah ameridhika nao nao wameridhika Naye. Na Amewaandalia mabustani ipitayo chini yake mito - ni wenye kudumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa." (09:100)**

## 03. BAADHI YA ALAMA ZA DA'WAH SALAFIYYAH

Mada ya leo ni kuelezea shubha na hoja tata zinazodaiwa na kupakiziwa Da'wah hii yenye kubarikiwa ya haki. Kwanza kabisa kabla sijaanza shubha na hoja hizi tata wanazozidai kwa Da'wah hii ya haki, napenda kuelezea alama kubwa za Da'wah hii ya haki.

Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amesema:

﴿قُلۡ هَٰذِهِۦ سَبِيلِيٓ أَدۡعُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا۠ وَمَنِ ٱتَّبَعَنِيۖ وَسُبۡحَٰنَ ٱللَّهِ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ ٱلۡمُشۡرِكِينَ﴾

**"Sema: "Hii ndio njia yangu, nalingania kwa Allaah juu ya elimu mimi na miongoni mwa anayenifuata. Utakasifu ni wa Allaah na mimi si katika washirikina."" (12:108)**

Wanasema maulamaa kuwa Aayah hii inaelezea alama za Da'wah hii ya haki. Aliposema (Subhaanah):

﴿قُلۡ هَٰذِهِۦ سَبِيلِيٓ﴾

**"Sema: "Hii ndio njia yangu."**

Katika mwanzo wa Aayah hii kuna alama za Da'wah hii ya haki ambayo ni uwazi. Da'wah hii ya haki katika moja ya alama zake ni kwamba ni Da'wah ambayo iko wazi. Haina siri. Haina jambo la siri. Haina mambo ya kufichwa[4]. Bali ni Da'wah ambayo iko wazi:

﴿قُلۡ هَٰذِهِۦ سَبِيلِيٓ﴾

**4.** Miongoni mwa alama za Hizbiyyuun na Ahl-ul-Bid'ah ni kwamba Da'wah zao haziwi wazi. Utawaona siku zote hawakosi mambo ya kufichaficha na mambo ya siri. Hili ni tofauti na Da'wah Salafiyyah ambapo Da'wah yao inakuwa wazi siku zote, inamkaribisha mkubwa na mdogo, waume kwa wake, tajiri na masikini, mwarabu na bedui na kadhalika. Kwa hiyo ndugu muislamu! Chunguza siku zote utapoona Da'wah ya watu au kundi fulani ina mambo ya kufichaficha, basi jua hapo kuna jambo na tahadhari.

Aliulizwa Allaamah Ahmad bin Yahyaa an-Najmiy (Rahimahu Allaah) kuhusiana na mifumo kama hii swali lifuatalo:

**Swali 43:** Kuwapeleka vijana sehemu ambazo hakuna wakazi ni katika mfumo wa al-Ikhwaan al- Muslimuun au mambo sio hivyo?

**Jibu:** Ndio, huu ni mfumo wao. Huwaambia kuwa wanaenda kusoma Qur-aan na mfano wa mambo kama hayo halafu wanawapeleka kwa siri usiku sehemu za mbali. Wanakaa huko na wanakuwa na Anaashiyd na mfano wa Bid'ah kama hizo.

**"Sema: Hii ndio njia yangu"**

Bi maana ni njia yangu iko wazi.

﴿ قُلۡ هَٰذِهِۦ سَبِيلِيٓ أَدۡعُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِۚ عَلَىٰ ﴾

**"Sema: "Hii ndio njia yangu: nalingania kwa Allaah juu ya elimu."**

Hii ni alama nyingine ya Da'wah hii ya haki.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) katika kuelezea uwazi wa Da'wah hii amesema:

**"Nimekuacheni njia nyeupe; usiku wake ni kama mchana wake. Hapotei kuacha njia hii isipokuwa mwenye kuangamia."**

Da'wah iko wazi. Usiku ni kama mchana. Anayeacha njia na mwongozo huu ni lazima ataangamia kwa maneno haya ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): **"Hapotei kuacha njia hii isipokuwa mwenye kuangamia."**[5]

---

= Nakumbuka takriban miaka kumi na mbili au kumi na tano iliyopita niliitwa kambini ambapo nikaulizwa kama ni sawa kwenda na watu wanaotoka baada ya swalah ya Ishaa kuelekea sehemu ya mbali ambapo wanadai kuwa wanasoma Qur-aan na wanafanya ibaadah huko. Nikawaambia wasitoke.

**Mosi:** Kwa sababu watu hawa wakiwa ni wakweli katika yale wanayodai na kwamba kweli wanataka ibaadah, basi walitakikana wakae msikitini.

**Pili:** Mimi nachelea lau watakuwa ni wengi na wana mtoto mchanga, huenda wakashawishiwa na shaytwaan na kukapitika yatayopitika.

Baadhi yao walinijia na wakanituhumu kuwa nasema hili na lile ambapo nikawaraddi na kuwaambia kuwa Salaf walikuwa wakikemea kutangamana na waasi na wakakubali hilo. Kuna ambao walikuwa wamekaa nyuma ya watu hao. Kitendo chao hichi ni cha makosa. Watu hawa wanafanya mambo haya kwa lengo la kusitiri na kuficha [mambo yao] na wanawadhihirishia wale wafuasi walio pamoja nao. Hawawezi wayakaweka wazi wanapokuwa mbele ya umati wa watu. Wanayafichua mbele ya ambaye wanamwamini tu. Tunamuomba Allaah atuongoze sisi na wao katika njia iliyonyooka na awafikishe watu wote katika yale anayoyapenda na kuyaridhia. (al-Fataawaa al-Jaliyyah, uk. 32-33)

**[5]** Ibn Maajah (43), al-Haakim (01/96) na Ahmad (04/126). Ni Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Silsilah as-Swahiyhah (02/648).

Kwa hiyo hii ni alama ya kwanza kwa Da'wah hii ya haki ya kwamba ina uwazi. Maneno Yake:

﴿عَلَىٰ بَصِيرَةٍ﴾

**"... juu ya elimu."**

Wanachuoni wamesema: "**Baswiyrah** ni daraja kubwa ya yakini."

Bi maana uhakika. Da'wah hii ni ya elimu. Wanachuoni wamechukua Aayah hii kwamba ni sharti mlinganizi awe na elimu kwa kile anachokilingania.

Kwa hiyo Da'wah hii iliyobarikiwa mtu haruhusiwi kufanya Da'wah hii isipokuwa awe na elimu kwa lile analolilingania. Sio elimu kwa mambo yote, hapana. Sina maana kwamba mwenye kulingania Da'wah hii ni lazima awe anajua kila kitu. Hapana! Ajue kile kitu anachokilingania. Kama analingania katika Tawhiyd anatakiwa ajue Tawhiyd ni nini na vigawanyo vyake. Kama analingania katika Fiqh anatakiwa ajue mambo na masuala ya Fiqh na yanayohusiana na Fiqh. Si kwamba mtu yoyote afanye Da'wah. Ni lazima mtu awe na elimu kwa lile analolilingania.

﴿قُلْ هَٰذِهِۦ سَبِيلِيٓ أَدْعُوٓا۟ إِلَى ٱللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا۠ وَمَنِ ٱتَّبَعَنِي ۖ وَسُبْحَٰنَ ٱللَّهِ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ﴾

**"Sema: "Hii ndio njia yangu: nalingania kwa Allaah juu ya elimu mimi na anayenifuata. Utakasifu ni wa Allaah - nami si miongoni mwa washirikina." (12:108)**

Kwa hiyo hizi ni alama mbili. Katika alama za Da'wah hii ya haki ambayo ni Da'wah ya as-Salafiyyah ni uwazi, kuwa na elimu na yakini.

Ama Da'wah nyinginezo ambayo si Da'wah hii ya haki wao wanamruhusu kila mtu afanye Da'wah.[6]

6. Mfano wa Da'wah hizo ni kama Da'wah ya Jamaa'at-ut-Tabligh ambapo wanamruhusu kila mmoja kulingania. Sivyo tu, bali lau kafiri atasilimu leo na akajiunga nao basi watamwambia apite mbele msikitini na atoe kalima na haya yameshuhudiwa sehemu nyingi tu ambapo wanawalazimisha wafuasi wao kutangulia mbele na kuzungumza. Ajabu iliyoje hii! Ni vipi mtu ameingia katika Uislamu leo ataenda mbele za watu na kuongea?!

Kwa sababu hii, na sababu nyenginezo nyingi tu ambazo ni kubwa kuliko hii, ndio maana wanachuoni wetu wa zama hizi wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa 'ah wametahadharisha kundi hili la kipotevu ambalo lina mrengo wa Suufiyyah.

Kila mtu anaruhusiwa kufanya Da'wah. Sawa awe ni mjinga au awe vipi anafanya Da'wah. Hizi ni Da'wah nyinginezo ambazo si za haki. Lakini Da'wah hii ya haki mtu haruhusiwi kufanya Da'wah isipokuwa awe anajua lile analolilingania. Hapo ndipo anaruhusiwa kufanya Da'wah.

---

Baadhi ya wanachuoni kuhusu Jamaa 'at-ut-Tabligh:

**1-** Mufti wa Saudi Arabia aliyetangulia na kichwa cha maqaadhiy na wa mambo ya Kiislamu Shaykh na Imaam Muhammad bin Ibraahiym Aalush-Shaykh (Rahimahu Allaah) amesema:

"Hakuna kheri yoyote kwenye jumuiya hii. Ni jumuiya ilio na Bid'ah na upotevu. Baada ya kusoma vijitabu vilivyoambatanishwa, tumekuta vina upotevu, Bid'ah na propaganda za kuabudu makaburi na shirki, jambo ambalo haliwezi kunyamaziwa. Hivyo basi - Allaah Akitaka - tutalikemea na kufichua upotevu wake na kuraddi batili zake." (Majmuu"-ul-Fataawaa war-Rasaa-il (01/267))

**2-** Muftiy wa Saudi Arabia aliyetangulia Shaykh na Imaam 'Abdul-Aziz bin Baaz (Rahimahu Allaah) amesema:

"Jamaa at-ut-Tabligh hawana upambanuzi katika 'Aqiydah. Haijuzu kutoka nao ikiwa mtu hana elimu na upambanuzi wa 'Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa ah ili mtu aweze kuwanasihi na kuwaelekeza na kushirikiana katika wema." (ad-Da'wah (1438) (1414-11-03)).

Amesema pindi alipoulizwa kama wanaingia katika mapote sabini na mbili [yatayoingia Motoni]:

"Ndio, wanaingia katika mapote sabini na mbili. Mwenye kwenda kinyume na "Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaaah anaingia katika mapote sabini na mbili." (as-Salafiyyah (07/47) (1422)).

**3-** Imaam na Muhaddith Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Jamaa at-ut-Tabligh haikujengwa juu ya mfumo wa Qur-aan, Sunnah na Salaf. Hivyo haijuzu kutoka nao..." (al-Fataawaa al-Imaaraatiyyah).

Mpaka hapa ndugu msomaji utakuwa umeona walivyosema wanachuoni wakubwa juu ya jamaa'at-ut- Tabligh. Usidanganyike na yale yaliyosemwa na mlinganizi mmoja mjinga muhubiri wa Vetenari, pasi na aibu na haya, akiwasifia Jamaa at-ut-Tabligh na kusema kuwa wao ndio wanaomfuata Mtume. Subhaan Allaah! Ni vipi unaweza kuthubutu kuwafadhilisha Jamaa at-ut-Tabligh juu ya Salafiyyuun?

﴿كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَٰهِهِمْ ۚ إِن يَقُولُونَ إِلَّا كَذِبًا﴾

**"Neno kubwa linalotoka midomoni mwao, Hawasemi isipokuwa uongo tu." (18:05)**

Mshairi anasema:

**Je, huoni kama unashusha Hadhi ya upanga**

**unaposema kuwa upanga una makali zaidi kushinda bakora**

Katika alama nyingine za Da'wah hii ya haki ni kuanza jambo muhimu zaidi kisha lililo muhimu. Da'wah hii iliyobarikiwa katika alama zake ni kwamba Da'wah inaanzia jambo lililo muhimu zaidi halafu ndio linakuja lile lililo muhimu na mengineo. Lakini muhimu zaidi ndio linalotangulizwa.

Hakuna kilicho muhimu sana katika Da'wah kushinda Tawhiyd. Tawhiyd maana yake ni **kumpwekesha Allaah kwa kumuabudu**. Ndio maana Da'wah hii mtaona katika kila msikiti wanapoenda kufanya Da'wah, basi wanaipa kipaumbele Tawhiyd na somo la 'Aqiydah. Wanalipa kipaumbele kwa sababu ndio muhimu zaidi na msingi wa masuala yote ya kila muislamu.

Msingi mkubwa wa muislamu ni Tawhiyd. Hilo ni kwa sababu ibaadah zake haziwezi kukubaliwa kama sio mpwekeshaji. Kwa hiyo Tawhiyd ndio msingi. Unapoanza kujenga nyumba siku zote unaanza msingi. Huanzi sakafu juu. Bali unaanza msingi. Ndio mfano wa Da'wah hii iliyobarikiwa. Inaanza msingi halafu ndio kunakuja vitu vingine mpaka sakafu.

Lakini utaona Da'wah nyingine, ambazo si Da'wah hii iliyobarikiwa, zinaanza juu sakafu. Ni jambo lisilo na shaka ukianza nyumba sakafu itaporomoka. Ndio maana Da'wah zingine zinaporomoka kwa sababu wanaanza mambo na wanaacha msingi.

Kwa hiyo msingi wa kila muislamu kujua ni Tawhiyd. Da'wah za Mitume wote walikuwa kwanza wanalingania Tawhiyd. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amesema:

﴿وَلَقَدۡ بَعَثۡنَا فِي كُلِّ أُمَّةٖ رَّسُولًا أَنِ ٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَٱجۡتَنِبُواْ ٱلطَّٰغُوتَۖ﴾

**"Hakika Tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake kwamba] kwamba: " Mwabuduni Allaah na jiepusheni na Twaaghuut [miungu ya batili]." (16:36)**

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِيٓ إِلَيۡهِ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدُونِ﴾

**"Hatukutuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimfunulia Wahy ya kwamba: "Hakika hapana Mola mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa mimi, hivyo Niabuduni."" (21:25)**

Kwa hiyo Tawhiyd ndio msingi. Ndio maana Da'wah hii as-Salafiyyah inalipa kipaumbele suala zima la Tawhiyd.

Watoto wanatakiwa kufundishwa Tawhiyd. Watu wazima kadhalika wanatakiwa wafundishwe Tawhiyd. Kwa sababu ndio msingi.

Al-Bukhaariy na Muslim wamepokea ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipompeleka Mu'aadh Yemen alimwambia:

**"Wewe unakwenda kwa Ahl-ul-Kitaab. Liwe jambo la kwanza utakalowalingania "hapana mola mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah.**[7]

Hii ni Tawhiyd. Kwa hiyo Tawhiyd ndio msingi.

Alama kubwa ya Da'wah hii ya haki ni kwamba wanaanza msingi huu wa Tawhiyd. Hawaanzi mambo ya Jihaad na mengineo. Bali inaanza Tawhiyd kwanza kwa kuwa ndio msingi. Halafu mambo mengine yanafuatia baada ya kuwa watu wameshajua Tawhiyd.

Kwa hiyo alama hizi tatu ndio alama za kwanza. Lakini hata hivyo si kwamba ndio alama zote za Da'wah hii ya haki. Bali hizi ni baadhi ya alama za Da'wah hii ya haki. Nazo ni zifuatazo:

**Ya kwanza:** Uwazi.

**Ya pili:** Elimu.

**Ya tatu:** Kulingania katika msingi ambao ni Tawhiyd.

---

**7.** Al-Bukhaariy (1458) na Muslim (19)

## 04. Shubha ya kwanza: KUWAFARIKISHA WAISLAMU

Shubha zinazodaiwa na kupelekewa Da'wah hii ya haki ni nyingi. Katika Shubha hizo wanazodai kwamba Da'wah hii ya as-Salafiyyah inafarikisha baina ya waislamu. Wanasema kuwa ni Da'wah ya kuwafarikisha waislamu. Waislamu wamekuwa na mfarakano mkubwa na wamekuwa hawapendani kutokana na Da'wah hii ya haki.

Sio kweli. Sio kweli kwamba Da'wah hii As-Salafiyyah ni Da'wah ya kufarikisha watu. Ni uongo. Bali hii ni Da'wah ya kukusanya watu na kuwaweka watu wawe pamoja katika Aqiydah, 'ibaadah na mfumo. Ni kujengea maneno Yake (Ta'ala):

﴿وَٱعْتَصِمُواْ بِحَبْلِ ٱللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُواْ﴾

**"Shikamaneni na kamba ya Allaah nyote na wala msifarikiane." (03:103)**

Kwa hiyo Da'wah hii ya haki inawahimiza waislamu kufuata Aayah hii na nyinginezo kwamba waislamu wawe pamoja na wawe kitu kimoja. Umoja ni nguvu. Lakini umoja wa haki ndio wenye nguvu, umoja wa mfumo, Aqiydah na ibaadah.[8] Huu ndio umoja ambao Da'wah hii As-salafiyyah inaulingania. Huu ndio umoja uliokusudiwa katika Aayah za Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala):

﴿وَٱعْتَصِمُواْ بِحَبْلِ ٱللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُواْ﴾

**"Shikamaneni na kamba ya Allaah nyote pamoja wala msifarikiane." (03:103)**

---

**8.** Kama alivyosema Shaykh wetu (Hafidhwahu Allaah) tunalingania katika umoja na tunatahadharisha mfarakano, lakini hata hivyo inahusiana na umoja wa 'Aqiydah, mfumo na mwelekeo mmoja. Vinginevyo hatuwezi kuwa na umoja na Ahl-ul-Bid'ah wadh-Dhwalaal na Hizbiyyuun kwa sampuli zao zote. Umoja aina hii hauwezi kufua dafu na katu hauwezi kufikia katika malengo. Bali itakuwa ni kama ule umoja wa mayahudi na manaswara ambapo Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amesema juu yao:

﴿تَحْسَبُهُمْ جَمِيعًا وَقُلُوبُهُمْ شَتَّىٰ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَعْقِلُونَ﴾

**"Utawadhania wameungana pamoja, kumbe nyoyo zao zimetofuatiana - hayo ni kwa kuwa wao ni watu wasiokuwa na akili." (59:14)**

"Amewaamrisha wawe kitu kimoja na kuwakataza kufarikiana."

Kwa hiyo Da'wah Salafiyyah inawaita watu na kuwalingania wawe kitu kimoja. Waislamu wanatakiwa wawe ni ndugu. Lakini udugu uwe katika 'Aqiydah na mfumo. Inahusiana na Aqiydah ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah zake na mfumo wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah zake. Hivi ndivyo Da'wah Salafiyyah inavyowalingania watu. Hailinganii mfarakano kabisa kwamba watu wafarikiane. Hapana! Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

**"Jilazimieni na al-Jamaa'ah na tahadharini na mfarakano. Kwani hakika shaytwaan yuko pamoja na mmoja na shaytwaan pamoja na wawili yuko mbali zaidi."** [9]

Hadiyth hii inahimiza na kuamrisha waislamu wawe pamoja.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

**"Allaah anaridhia kwenu mambo matatu na anachukia mambo matatu; anaridhia kwenu kumuabudu Yeye peke yake na wala msimshirikishe Yeye na chochote, mshikamane na kamba ya Allaah nyote na wala msifarikiane na muwanasihi wale ambao Allaah amewatawalisha mambo yenu."** [10]

Haya ni mambo matatu ambayo Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) anayaridhia kwetu. Katika mambo haya ametaja:

﴿وَٱعۡتَصِمُواْ بِحَبۡلِ ٱللَّهِ جَمِيعٗا وَلَا تَفَرَّقُواْۚ﴾

**"Shikamaneni kamba ya Allaah nyote na wala msifarikiane." (03:103)**

Kwa hiyo Da'wah Salafiyyah inahimiza watu washikamane na kamba ya Allaah na wasifarikiane. Kwa sababu kufarikiana si katika ada ya waislamu wala si katika mwenendo wa waislamu. Bali ni katika mwenendo wa Ahl-ul- Kitaab. Amesema (Ta'ala):

---

= Shaykh-ul-Islaam amesema: "Bid'ah zimefungamanishwa na mfarakano (Furqah) na Sunnah imefungamanishwa na mkusanyiko (Jamaa ah). Ndio maana kunasemwa Ahl us Sunnah wal-Jamaa ah na Ahl-ul-Bid'ah wal Furqah."
(al- Istiqaamah (01/41))

**9.** Abu Daawuud (4607) na At-Tirmidhiy (2676). **10.** Muslim (1715).

﴿وَلَا تَكُونُواْ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ۝ مِنَ ٱلَّذِينَ فَرَّقُواْ دِينَهُمْ وَكَانُواْ شِيَعًاۖ كُلُّ حِزْبِۭ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ﴾

**"Msiwe katika washirikina - wale ambao wamefarikisha dini yao na wakawa makundi makundi. Kila kundi kwa yaliyonayo linafurahia." (30:31- 32)**

Jambo la kufarikiana sio la waislamu. Waislamu si ada yao kufarikiana. Waislamu Kitabu chao ni kimoja, Allaah ni mmoja, Mtume wao ni mmoja na Hadiyth ni hizi hizi za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

Lakini waislamu kwa vile hawafuati Aayah na Hadiyth hizi za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndio wamefarikiana katika Aqiydah, mfumo, ibaadah, mu'amala na katika kila jambo waislamu wamefarikiana. Sasa Da'wah Salafiyyah inawaleta waislamu wawe kitu kimoja katika masuala haya; katika mfumo, 'Aqiydah, 'ibaadah na mu'amala na mambo mengine ya dini. Da'wah Salafiyyah haifarikishi. Ni uongo kwamba Da'wah Salafiyyah inalete mpasuko kati ya waislamu. Huu ni uongo:

﴿كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَٰهِهِمْۚ إِن يَقُولُونَ إِلَّا كَذِبًا﴾

**"Neno kubwa linalotoka midomoni mwao. Hawasemi isipokuwa uongo tu." (18:05)**

Kwa hiyo Da'wah Salafiyyah ni Da'wah ambayo inataka kuwakusanya waislamu wawe kitu kimoja. Sio Da'wah yenye kufarikisha kabisa. Hilo ni kutokana na Aayah za Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) na Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

## 05. Shubha ya pili: WANA MSIMAMO MKALI

Wanasema kuwa Da'wah Salafiyyah ina ugumu[11] na kupetuka mipaka,[12] Maulamaa wanasema:

"Ugumu unapatikana katika moja ya mambo mawili:

**La kwanza:** Kumuabudu Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kwa ibaadah ambazo Allaah hakuziteremshia dalili zozote.

**La pili:** Kupetuka mipaka katika dini."

Huu ndio ugumu. Ukiangalia katika uwanja wa Da'wah utaona kwamba Ahl- us-Sunnah wal-Jamaah hawana ibaadah ambazo hazina dalili. Ukija katika kumuabudu Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kwa ibaadah ambazo Allaah hakuziteremshia dalili, Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa ´ah wanamuabudu Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kwa ibaadah alizoweka Mwenyewe. Hawajazidisha katika mambo ya ibaadah kwa sababu ya Hadiyth ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

**"Mwenye kuzua katika dini yetu hii lisilokuwemo, jambo hilo litarudishwa [litakataliwa]."**[13]

Katika upokezi mwingine imekuja:

**"Mwenye kufanya amali ambayo haiko katika dini yetu, amali hiyo itarudishwa [itakataliwa]."**[14]

Kwa hiyo Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah hawajaongeza ibaadah yoyote wala jambo lolote la kumuabudu Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala). Wanamuabudu Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kwa 'ibaadah zile zile alizofundisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Hii ndio muqtadha Wa ninashuhudia ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah.

---

**11.** Tashaddud.

**12.** Ghuluu

**13.** Al-Bukhaariy (2697) na Muslim (18) na (1718).

**14.** Muslim (18) na (1718).

Muqtadha wake ni: kumtii katika yale aliyoamrisha, kumsadikisha katika aliyoelezea, kujiepusha na yale aliyokataza na kukemea na kutomuabudu Allaah isipokuwa kwa yale Aliyoweka.

Huu ndio mfumo wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah. Wao hawamuabudu Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kwa ibaadah yoyote ambayo hakuiweka Yeye au Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Hudhayfah bin al-Yamaan (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye alikuwa muweka siri [wa Mtume] amesema:

"Ibaadah yoyote ambayo hawakufanya Maswahabah wa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), na nyinyi msiifanye."

Bi maana ibaadah hiyo itakuwa haifai. Huu ndio mfumo wetu wa Ahl-us- Sunnah wal-Jamaa 'ah. Inahusiana na 'ibaadah zile zile alizozifundisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Hatuongezi mambo mengine. Lakini upande mwingine ukiangalia Ahl-ul-Bid'ah wana mambo na Bid'ah nyingi walizoziongeza katika dini. Wanamuabudu Allaah kwa Bid'ah. Hayastahiki kuitwa ibaadah. Wameongeza Bid'ah nyingi na wamezifanya kwamba ni ibaadah. Wana ziara za ki-Bid'ah. Leo hivi watu wako katika ziara za ki- Bid'ah. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) hakuteremshia dalili yoyote juu ya ziara hizi za ki-Bid'ah. Moja wapo ni Maulidi. Kuna mambo mengi sana ya ki- Bid'ah wameyazusha.[15]

---

**15.** Hakika ni jambo lisilokuwa na shaka yoyote kuwa kusherehekea mazazi ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ni Bid'ah na upotevu. Wanachuoni wetu wa Ahl us Sunnah wal Jamaa'ah, sawa wa kale na wa sasa, wametunga vitabu vikubwa na vidogo juu ya hilo wakiyatahadharisha. Hilo ni kwa sababu ni jambo halikufanywa na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), Maswahabah wake, Taabi'uun na waliokuja baada ya Taabi'uun. Bali ni mambo yalizuliwa na Faatwimiyyuun Ubaydiyyuun ambao ni Shiy ah wa huko Misri waliojitokeza baada ya karne bora zilizosifiwa na Mtume ('alayhis-Swalaatu was- Salaam).

**Kidokezo**! Hii ni miongoni mwa shubha nyingine inayotumiwa na wazushi wengi kwamba Salafiyyuun hawampendi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Huu ni uongo mkubwa kabisa uliokubuhi na kupindukia. Mshairi anasema:

*Je, unamuasi mpenzi wako na wewe unadai kumpenda?!*
*hakika hili ni jambo la kushangaza kweli kweli*
*Lau mapenzi yako yangelikuwa ya kweli basi ungelimtii*
*hakika mpenzi kwa ampendae humitii*

Kwa hiyo haya madai ya ugumu yanafaa warushiwe wao Ahl-ul-Bid'ah na kwamba wao ndio wana ususuwavu. Hilo ni kwa sababu wanamuabudu Allaah kwa ibaadah ambazo Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) hakuziweka Mwenyewe wala Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Kwa hiyo madai ya ususuwavu yanafaa wapewe wao Ahl-ul-Bid'ah.

Ugumu pia unakuja katika kupetuka mpaka katika dini. Hii ndio maana ya ususuwavu. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amesema:

﴿يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ لَا تَغۡلُواْ فِي دِينِكُمۡ وَلَا تَقُولُواْ عَلَى ٱللَّهِ إِلَّا ٱلۡحَقَّۚ﴾

**"Enyi Ahl-ul-Kitaab! Msipindukie mipaka katika dini yenu wala msiseme juu ya Allaah isipokuwa ukweli." (04:171)**

Mayahudi na manaswara wamepetuka mpaka katika dini. Manaswara wamepetuka mpaka kwa 'Iysaa. Mayahudi wamepetuka mpaka kwa 'Uzayr:

﴿وَقَالَتِ ٱلۡيَهُودُ عُزَيۡرٌ ٱبۡنُ ٱللَّهِ وَقَالَتِ ٱلنَّصَٰرَى ٱلۡمَسِيحُ ٱبۡنُ ٱللَّهِۖ﴾

**"Na mayahudi wanasema:"Uzayr ni mwana wa Allaah" na manaswara wanasema: "al-Masiyh ni mwana wa Allaah." (09:30)**

---

= Kidhibiti cha kumpenda Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), kama walivyosema wanachuoni, ni kile alichokitaja Allaah (Ta'ala) pale aliposema

﴿قُلۡ إِن كُنتُمۡ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِي﴾

**"Sema [Mtume uwaambie]: "Mkiwa mnampenda Allaah, basi nifuateni mimi." (03:31)**

Baadhi ya maimamu na wanachuoni wakubwa walioandika wakiraddi Bid'ah hii ni wafuatao:

**1-** Imaam Abu Hafsw Taj-ud-Diyn al-Faakihaaniy (aliyefariki. 734) katika kitabu chake "al-Mawrid fiy 'Amal-il-Mawlid"

**2-** Shaykh-ul-Islaam Ahmad bin Taymiyyah katika "Iqtidhwaa' as Swiraatw al-Mustaqiym (02/123-124)

**3-** Imaam 'Abdul-Aziyz bin Baaz katika "Fataawaa Ulamaa al-Balad al-Haraam", uk. 467 na "Fataawaa Arkaan-il-Islaam" uk. 109-110

**4-** Imaam Muhammad bin Swaalih bin Uthaymiyn katika "Fataawaa 'Ulamaa al-Balad al-Haraam", uk. 462-464

**5-** Mwanachuoni Muqbil bin Haadiy al-Waadi iy katika "Tuhfat ul Mujiyb" uk. 62-63

**6-** Mwanachuoni Swaalih bin Fawzaan al-Fawzaan katika kitabu chake cha kipekee "Hukm-ul-Ihtifaal bil- Mawlid an-Nabawiy"

Huku ni kupetuka mpaka katika dini. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amekataza jambo la kupetuka mpaka katika dini pale aliposema:

**"Msipetuke mpaka katika kunisifu kama walivyopetuka mpaka wakristo kwa Issa bin Maryam wakasema ni mwana wa Allaah. Hakika mimi si jengine bali ni mja. Hivyo semeni "Mja wa Allah na Mtume wake."**[16]

Hapa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anakataza kupetuka mpaka katika kumsifu. Kwa hiyo Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah hawana jambo la kupetuka mpaka.

Upande mwingine ukiangalia Ahl-ul-Bid'ah wana jambo la kupetuka mpaka. Wamemsifu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) zaidi ya mpaka wake. al-Buuswiyriy ambaye ni Suufiy amesema katika ubeti wake wa al-Burdaa:

*Hakika ni katika ukarimu wako ulimwengu na Aakhirah*
*Na katika elimu zako ni elimu ya Ubao na kalamu*

maana Ubao uliohifadhiwa.[17]

Ibn Rajab al-Hanbaliy amesema:

**"Ikiwa ulimwengu na Aakhirah vyote viwili ni vya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), basi hakumuachia Allaah kitu chochote."**

Shaykh Ibn 'Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) amesema kuhusu ubeti huu wa al-Buuswiyriy:

**"Huyu amemfanya Mtume ni zaidi ya Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala)."**

Huu ndio ugumu. Kwa hiyo sifa ya ususuwavu Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wametakasika nayo kabisa. Ahl-us-Sunnah hawana ugumu katika dini.

---

= Kadhalika kuhusiana na masuala haya usihadaike na muhubiri wa Vetenari ambaye katika moja ya mikanda yake nimemsikia akisema kwamba haitakikani kwa waislamu kukatana, kuchukiana na kuhamana juu ya masuala kama haya yaani akimaanisha kusherehekea Maulidi - na akaashiria kwamba ni kama tofauti zingine zilizo kati ya wanachuoni wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa ah kama mfano wa Qunuut ya Fajr na mengineyo. Ni nani aliyekutangulia kusema maneno kama haya? Allaah akuongoze wewe na sisi.

**16.** Al-Bukhaariy (3445).

**17.** Lawh-un-Mahfuudhw. Hii ni moja kati ya Qaswiydah maarufu sana na mara nyingi inasomwa mfungo sita (Rabiy al-Awwal) katika sherehe za Maulidi.

Baadhi ya Maswahabah walikwenda kwa wake zake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuulizia ibaadah za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) za siri alizokuwa akifanya nyumbani kwake. Wakaenda kuulizia kwa wake za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambapo wakawa wameelezewa. Walipoelezewa wakaziona kama ni ibaadah chache zile anazofanya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Mmoja katika Maswahabah zake akasema: "**Mimi nitafunga milele sifungui**." Mwingine akasema: "**Mimi nitafanya ibaadah usiku mzima silali**." Mwingine akasema: "**Mimi sitaoa wanawake**." Anasema kuwa atakaa hivi hivi bila ya kuoa kwa sababu wanawake hawa wanashawishi. Wakati wa 'ibaadah mwanamke anakushikashika na kukuvuta. Akasema kuwa yeye hatooa kabisa. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipoelezewa suala lile akawakusanya Maswahabah (Radhiya Allaahu 'anhum) na kuwakataza jambo hilo. Akawaambia:

**"Mimi ni mchaji wenu zaidi kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala). Lakini mimi nafunga na nafungua, naswali usiku na nalala na naoa wanawake. Atakayeichukia Sunnah yangu si katika mimi."**[18]

Akawaambia hayo wanayoyafanya ni ugumu na kupetuka mpaka. Haitakiwi katika dini. Kupetuka mpaka na utawa hautakiwi katika dini kwamba huoi mwanamke kwa sababu unafanya ibaadah sana na unataka kumuabudu Allaah sana usiku na hivyo ukawa hutaki kuoa! Huko ndiko kupetuka mpaka. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akawakataza.

Kwa hiyo Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah wanakataza mambo haya. Hii inamaanisha kwamba hakuna kupetuka mpaka katika Da'wah Salafiyyah na ugumu. Kupetuka mpaka ni mambo yao Ahl-ul-Bid'ah. Ugumu ni mambo yao ya Ahl-ul-Bid'ah. Ususuwavu ni mambo yao Ahl-ul-Bid'ah. Sio mambo ya Ahl-us-Sunanh wal-Jamaa'ah.

---

**18.** Muslim (1401) na an-Nasaa iy (3217).

## 06. Shubha ya Tatu: SALAFIYYAH NI KIPOTE NA KUJIITA "SALAFIY" NI KUJITAKASA

Shubha nyingine inayopakaziwa kwa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni kwamba Salafiyyah ni kipote kama vipote vingine vya ki-Bid'ah. Wanasema kuwa Salafiyyah ni kikundi kama vikundi vingine vya ki-Bid'ah. Wanasema pia kuwa kujiita Salafiyyah ni kujitakasa na wanasema kwamba Salafiyyuun wanajitakasa na wanaona kuwa wao ni wasafi. Hii ni shubha nyingine ambayo inapakaziwa Da'wah hii.

Maimamu wa Salafiyyuun wanasema:

**"Salafiyyah ni kundi. Lakini ni kikundi cha Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala**). Amesema (Ta'ala):

﴿ أَلَآ إِنَّ حِزْبَ ٱللَّهِ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ﴾

**"Tanabahi! Hakika kundi cha Allaah ndio lenye kufaulu"[19](58:22)**

Kwa hiyo ni kweli kwamba ni kikundi. Lakini si kama vikundi vingine vya ki-Bid'ah. Hiki ni kikundi cha Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala). Ni kikundi kitakachookoka na Moto. Hilo ni kutokana na Hadiyth ya mfarakano ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam);

---

**19.** Miongoni mwa waliosema hivo ni 'Allaamah Swaalih al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah). Aliulizwa swali lifuatalo:

**Swali:** Je, Salafiyyah ni kipote (Hizb) na inajuzu...?

**Jibu:** Salafiyyah ndio asli na sio kipote. Ndio asli. Ndio asli na yote yenye kwenda kinyume nayo ni batili. Ni kweli kwamba kinaweza kuitwa Hizb kwa sababu Allaah anasema:

﴿ أُوْلَٰٓئِكَ حِزْبُ ٱللَّهِۚ ﴾

**"Hao ndio kundi la Allaah." (58:22)**

Tunasema kuwa ni kweli kwamba ni kikundi, lakini ni kundi la Allaah. wenye kwenda kinyume na kundi hilo ni kundi la Shaytwaan, kama alivyosema Allaah:

﴿ أُوْلَٰٓئِكَ حِزْبُ ٱلشَّيْطَٰنِۚ ﴾

**"Hao ndio kundi la shaytwaan." (58:19)**

Ama kusema tu kuwa Salafiyyah ni kipote halafu ukanyamaza, si sawa. Salafiyyah ni kundi la Allaah kwa sababu Allaah amewaita kuwa ni "kundi la Allaah". (Sahab.net)

**"Mayahudi wamefarikiana vikundi sabini na moja. Wakristo wamefarikiana vikundi sabini na mbili. Ummah huu utafarikiana vikundi sabini na tatu. Vyote vitakwenda Motoni isipokuwa [kikundi] kimoja." Maswahabah wakamuuliza: "Ni kikundi gani, ee Mtume wa Allaah?" Akasema: "Ni al- Jamaa'ah."**[20]

Kikundi hicho ni al-Jamaa´ah ambayo inafuata mfumo huu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake. Kundi hili moja ndilo linalofuata Aqiydah ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake. Katika upokezi mwingine imekuja:

**"Ni kikundi ambacho kiko katika mfano wa nilivyo mimi hii leo na Maswahabah wangu."**[21]

maana ni kikundi kitakachofuata mfumo wangu mimi na Maswahabah wangu. Hiki ndicho kikundi kilichookoka na kipote kilichonusuriwa. Kwa hiyo Salafiyyah ni kikundi. Lakini ni kikundi kilichookoka. Sio hivi vipote alivyosema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

**"Vyote vitakwenda Motoni isipokuwa [kikundi] kimoja."**

Ndugu zangu waislamu! Jengine ni kuwa kujiita "Salafiy" sio kujitakasa[22] Mtu akijiita "Salafiy" ni kwamba anajibasibisha na watu wema waliotangulia

---

**20.** Ibn Maajah (3992).

**21.** Abu Daawuud (4597) na Ahmad (04/102).

**22.** Shaykh-ul-Islaam amesema yafuatayo:

"Hakuna aibu kwa yule mwenye kudhihirisha madhehebu ya Salaf, akajinasibisha nayo na akarejea kwayo. Bali ni wajibu kumkubalia hilo kwa makubaliano kwa sababu madhehebu ya Salaf si jengine isipokuwa ni haki." (Majmuu-ul-Fataawaa (04/149))

Imaam adh-Dhahabiy amesema kuhusu Muhammad bin Muhammad al Bahraaniy:

"Alikuwa ni mtu wa dini, mwema na Salafiy." (Mujaam-ush-Shuyuuk (02/280))

Amesema kuhusu Ahmad bin Ahmad bin Ni'mah al-Maqdisiy:

"Alikuwa ni mwenye kushikamana na Aqiydah ya Salaf." (Mujaam ush-Shuyuukh (01/34))

Aliulizwa Mwanachuoni Ahmad bin Yahyaa an-Najmiy (Rahimahu Allaah) kuhusiana na masuala haya swali lifuatalo:

**Swali 04:** Je, kuna Salafiyyah ya zamani na Salafiyyah mpya au kuna Salafiyyah moja peke yake?

**Jibu:** Salafiyyah ni moja peke yake. Anayedai kuwa kuna Salafiyyah ya zamani na Salafiyayh mpya amesema uongo

Maana yake ni kwamba mimi najinasibisha na watu wema waliotangulia. Kama nilivyosema ya kwamba ni Maswahabah, Taabi'uun na waliokuja baada ya Taabi'uun. Kujinasibisha na watu hawa itakuwaje kwamba ni kitu kibaya? Vipi kujinasibisha na Maswahabah itakuwa ni kitu kibaya hakifai? Vipi ni kujitakasa? Bali Shaykh Ibn Baaz (Rahimahu Allaah) alipoulizwa juu ya hili akasema:

**"Ndio, ni kujitakasa. Huku ni kujitakasa kwa lazima."**[23]

Kujinasibisha na Maswahabah (Radhiya Allaahu 'anhum) ni kujitakasa kwa lazima. Kila muislamu anawajibika kujinasibisha na Maswahabah kwa kuwa ndio watu bora baada ya mitume wa Allah na watu waliosifiwa na Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

**Ndugu zangu waislamu!** Kila muislamu anawajibika kufuata mwongozo huu. Kila muislamu anawajibika kufuata mfumo huu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake. Akishafuata mwongozo huu na mfumo huu anajinasibisha na hao watu wema. Hajinasibishi na mwengine. Asipojinasibisha na hao watu wema ajinasibishe na nani? Kwa hiyo ni kujitakasa kwa lazima kujiita "mimi ni Salafiy".

---

= Lau tutatazama juu ya 'Aqiydah ya Salaf, kuanzia wakati wa Maswahabah mpaka hii leo, basi tutaona kuwa Aqiydah ni moja. Haitofautiani kamwe, hata kama watatofautiana katika mambo madogo madogo ambayo hayahusiani na misingi. Wanatofautiana katika mambo madogo madogo. Pamoja na hivyo hawaashiriani vidole kwa hayo. Hii ndio njia ya Maswahabah (Radhiya Allaahu 'anhum). Ama inapokuja katika 'Aqiydah, mfumo wao ni mmoja tangu wakati wa Maswahabah mpaka hii leo." (al-Fataawaa al- Jaliyyah, uk. 09)

**23.** Fatwa hiyo ni hii ifuatayo ambapo aliulizwa Imaam 'Abdul-Aziyz bin Baaz (Rahimahu Allaah) ifuatavyo:

"Unasemaje kuhusiana na mwenye kujiita "Salafiy" au "Athariy"? Je, ni kujisifu?

Akajibu (Rahimahu Allaah):

"Haina neno ikiwa kama kweli ni Athariy au Salafiy. Kama mfano wa jinsi baadhi wakisema fulani ni "Salafiy" na "Athariy". Sifa kama hii ni lazima. Ni sifa ya lazima." (Kutoka kwenye mkanda "Haqq-ul-Muslim" 1413/01/16 Twaait)

## 07. Shubha ya Nne: ALLAAH AMETUITA WAISLAMU

Katika shubha wanasema kuwa Allaah (Subaanahu wa Ta'ala) amewaita watu wote "waislamu":

﴿هُوَ سَمَّىٰكُمُ ٱلْمُسْلِمِينَ مِن قَبْلُ وَفِى هَـٰذَا﴾

**"Yeye ndiye amekuiteni waislamu huko nyuma na hivi sasa." (22:78)**

Wanauliza ni kwa nini sisi tunajiita Salafiyyuun. Wanasema kuwa twatakiwa kujiita "waislamu" tu kama watu wengine. Hii nayo ni shubha nyingine.

Wanazuoni wanasema: Ni kweli Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amewaita waislamu. Lakini ni wakati ule ambapo hakuna Bid'ah yoyote. Allaah aliwaita waislamu jina hilo wakati ule ambapo hakuna Bid'ah, hakuna wapindaji, Hizbiyyuun na wazushi wowote. Hapo ndipo Allaah aliwaita waislamu. Sasa hivi baada ya kutokea vikundi vingi na tofauti nyingi ni lazima kuna watu wajiite Salafiyyuun ili kuepukana na watu wale wa Bid'ah. Amesema (Ta'ala):

﴿وَكَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ ٱلْـَٔايَـٰتِ وَلِتَسْتَبِينَ سَبِيلُ ٱلْمُجْرِمِينَ﴾

**"Na hivyo ndivyo Tunavyopambanua Aayah na ili idhihirike njia ya wahalifu." (06:55)**

Malengo ni ili ijulikane na ibainike njia ya wahalifu ndio maana ni lazima watu wajiite Salafiyyuun. Lengo ni ili kuwe na upambanuzi baina yao na wengine. Kwa sababu Shiy'iy anajiita muislamu, Qaadiyaaniy[24] anajiita muislamu. Sijui nani anajiita muislamu. Sasa sisi na Shiy'ah sote ni waislamu? Haiwezekani. Ni lazima tujipambanue. Ni lazima tujinasibishe na watu wema waliotangulia ili tupambanukane na hawa waongo.

---

**24.** Qaadiyaaniyyah ambao vilevile wanaitwa "Ahmadiyyah". Ni kipote kinachomfuata Mirzaa Ghulaam Ahmad al-Qaadiyaaniy na wanaamini kuwa ndiye Mtume baada ya Muhammad bin 'Abdillaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Kwa ajili hiyo wanachuoni wote wa leo wameafikiana juu ya ukafiri wa pote hili. Kujengea juu ya haya napenda kutumia fursa hii kuwatahadharisha ndugu zetu waislamu juu ya kikundi hichi kwani kimeanza kuenea kwa kasi huko Kenya na Tanzania. Atayeingia katika uislamu wa kikadiyani hakuna tofauti na aliyetoka katika Uislamu na kuingia katika Ukristo, Uyahudi na dini nyenginezo za kikafiri.

Amesema (Ta'ala):

﴿لِيَمِيزَ ٱللَّهُ ٱلْخَبِيثَ مِنَ ٱلطَّيِّبِ وَيَجْعَلَ ٱلْخَبِيثَ بَعْضَهُۥ عَلَىٰ بَعْضٍ فَيَرْكُمَهُۥ جَمِيعًا فَيَجْعَلَهُۥ فِى جَهَنَّمَ﴾

**"Ili Allaah apambanue waovu na wema kisha aweke waovu juu ya waovu wengine, kisha awavugumize pamoja awatie Motoni." (08:370)**

maana:

Ni lazima kuwe na upambanuzi. Da'wah Salafiyyah ni lazima iwe na upambanuzi. Salafiyyuun wanajipambanua na wazushi. Ndio Salafiyyuun hawaruhusiwi kukaa na hawa wazushi na kushirikiana nao kwa ajili kupatikane upambanuzi.

Kwa hiyo hii ni Shubha nyingine ambayo inapakaziwa Da'wah Salafiyyah. Wanasema ni kwa nini wanajiita Salafiyyuun ilihali watu wengine [wote] wanajiita waislanu. Ni kwa nini wasijiite waislamu tu?

Kwa hiyo ndugu zangu waislamu kuna Shubha nyingi zinazonasibishwa katika Da'wah hii as-Salafiyyah.

## 08. Shubha ya Tano: WALINGANIZI WA SALAFIYYAH NI WAKALI

Wanasema kuwa wale walinganizi wa Da'wah Salafiyyah ni wakali. Wanasema kuwa walinganizi wa Da'wah Salafiyyah ni wakali kama masimba. Ukali wao ni kama chui na pindi wanapotoa Khutbah macho yanakuwa mekundu na hawachekicheki katika Khutbah. Wanasema kuwa wanatakiwa wachekecheke kidogo na wawe lainilaini.

Hii ni shubha nyingine ambayo inapakaziwa Da'wah Salafiyyah. Wanasema kwamba walinganizi ni wakali na wanafukuza watu katika Da'wah kwa sababu ya ukali wao.[25] Ukiuliza huo ukali ni aina gani na ni maneno gani wanayosema mpaka mseme kuwa ni wakali? Wanasema kuwa Da'wah yao inakataza watu kunyoa ndevu.[26] Da'wah yao inakataza wanaume kupeana mkono na wanawake.[27] Da'wah inakataza wanaume wasivae nguo ndefu.[28] Huu ndio ukali!!! Kukataza watu wasinyoe ndevu eti ndio ukali!!! Basi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndiye aliyeanza ukali huo. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndiye aliyeanza ukali huu sisi tukafuatia. Sisi tunamuigiza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

---

**25.** Shubuha hii aliiraddi Mwanachuoni Rabiy bin Haadiy al-Madkhaliy (Rahimahullaah) kiutaalamu na kiufundi wa hali ya juu katika mkanda ulio na kichwa cha khabari "ar-Radd 'alaa man yaswif us Salafiyyiyn bish-Shiddah". Ninamshauri kila mwanafunzi autafute mkanda huo na ausikize.

**26.** Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndiye alikuwa wa kwanza kuwaamrisha wanaume kufuga ndevu pale aliposema:

**"Ziacheni ndevu"** al-Bukhaariy (5893), Muslim (259) na an-Nasaa 'iy (5226).

**27.** Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndiye alikuwa wa kwanza kutopeana mikono na wanawake wasiokuwa Mahram zake. 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) amesema:

**"Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hajapatapo kugusa mkono wa mwanamke hata siku moja."** al-Bukhaariy (7214).

**28.** Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndiye alikuwa wa kwanza kuelekeza katika kitendo hichi na akamkemea mwanaume mwenye kufanya hivo kwa kusema:

**"Kilichoko chini ya nguyu mbili za miguu ni Motoni."** al-Bukhaariy (5787), an-Nasaa iy (5331) na Abu Daawuud (4093).

Sasa kama kweli Salafiyyuun ni wakali kwa sababu ya kuwahimiza watu mambo haya na mfano wa haya je, ukali huu wameuanza wao au ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndiye kauanza?!

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

**"Fugeni ndevu."**

**"Ziacheni ndevu."**

**"Wakhalifuni waabudu moto."**

**"Wakhalifuni Mayahudi."**[29]

Kumekuja matamshi mbalimbali ya Hadiyth.

Wanasema eti huo ndio ukali. Wanaume ndio wameambiwa wafuge ndevu na wala si wanawake. Wanaume tumewaambia wafuge ndevu kama alivyowaamrisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Sasa huu ndio ukali!!! Tunaambiwa twafukuza watu kwa sababu tumewaambia wanaume wafuge ndevu badala ya kuwaambia "Aa nyoeni!". Wanasema msiwaambie fugeni ndevu namna hiyo waachieni. Kidogo, kidogo. Eti mpaka sasa watu waambie "Pole! Pole na Da'wah!" Huu ni mwaka wa ishirini twafanya Da'wah twaambiwa pole pole. Watu wengine wafa, walinganizi wengine wafa na watu wanaolinganiwa wafa. Watu wasiambiwe mambo waliyoamrishwa na Mtume na wala wasikatazwe makatazo ya Mtume. Waaachiwe tu kidogo kidogo poleni poleni jamani taratibuni. Utaratibu gani huu? Mpaka lini? Wanataka tuwape muda mpaka lini? Nyinyi mnaotwambia kuwa twende taratibu na Da'wah yetu na kwamba tunaenda mbio sana na tena kwa spidi kubwa ya Da'wah, twambie [wewe] spidi ndogo ni ipi na inakuwa kwa miaka mingapi mpaka tusikuamrishe wewe usinyoe ndevu.

Ndugu zangu waislamu! Sio ukali. Haya ni maamrisho ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), **"tuwakhalifu mayahudi"** kwa kuwa wao wananyoa ndevu hivyo sisi tusinyoe. Ndevu ni pambo la mwanaume. Pambo la mwanaume ni kuwa na ndevu. Kadhalika mwanaume hatakiwi kuteremsha nguo yake na kuburuta. Hii si sifa ya mwanaume. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anasema: **"Nguo ilio chini ya tindi mbili za miguu [mtu] ni Motoni."**[30]

---

**29.** 29 al-Bukhaariy (5893), Muslim (259) na an-Nasaa 'iy (5226).

**30.** al-Bukhaariy (5787), an-Nasaa 'iy (5331) na Abu Daawuud (4093).

Sasa tusiwatahadharishe watu na Moto? Tuwaachie watu tu wafanye watakavyo? Da'wah itakuwa vipi hivyo? Tusiwaamrishe watu mema na tusiwakataze maovu kwa vile twaambiwa ni wakali na kwamba watu watakimbia. Haya wakimbie! Hizi ni Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na si zetu.

Watu waachiwe tu waimbe maredioni na watoe CD za nyimbo.[31] Bado tuwaache tu na tusiwakataze nyimbo na tusikataze watu kusikiliza nyimbo.[32] Tukikataza watu twaambiwa kuwa sisi ni wakali.

---

**31 na 32.** "Mwanachuoni Swaalih al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema hali ya kukemea na kukaripia Bid'ah hii ifuatavyo:

"Kitu ambacho inatakikana kukisisitiza ni yale ambayo vijana wengi wenye dini wametumbukia ndani yake. Wanasikiliza Anaashiyd zinazoimbwa kwa sauti za pamoja na wanaziita kuwa ni "**Anaashiyd za Kiislamu**". Ni aina ya nyimbo na wakati mwingine zinaimbwa kwa sauti zenye kufitinisha. Mikanda hii inauzwa pamoja na mikanda ya Qur-aan na mihadhara ya dini. Anaashiyd hizi kuziita kuwa ni "**Anaashiyd za din**i" ni makosa. Kwa sababu Uislamu haukutuwekea Anaashiyd. Kinyume chake umetuwekea kumdhukuru Allaah, kusoma Qur-aan, kujifunza elimu yenye manufaa na kadhalika.

Kuhusiana na Anaashiyd ni katika dini ya Suufiyyah iliyozushwa. Wameifanya dini kuwa ni pumbazo na mchezo. Kuzifanya Anaashiyd ni katika dini ni jambo limeshabihiana na manaswara ambao dini yao wameifanya nyimbo na sauti za pamoja.

Lililo la wajibu ni kutahadhari na Anaashiyd hizi na kupiga marufuku kuuzwa na kusambazwa. Isitoshe Anaashiyd hizi zinaweza kuchochea katika hamasa zenye fitina na uchochezi kati ya waislamu.

Wanaeneza Anaashiyd hizi kwa kutumia hoja ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alikuwa anaweza kusomewa mashairi na akasikiliza na kuzikubali. Jibu ya hilo ni kwamba mashairi yaliyokuwa yakisomwa kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hayakuwa yanasomwa kwa sauti za pamoja kwa sampuli ya nyimbo. Vilevile hayakuwa yanaitwa "ya Kiislamu". Ilikuwa ni mashairi ya kiarabu yaliyo ndani yake na hekima, methali, ujasiri na ukarimu. Maswahabah walikuwa kila mmoja akiyasoma kivyake kutokana na maana yaliyokuwa nayo. Walikuwa wanaweza kusoma mashairi wakati wanapofanya kazi za nguvu kama ya ujenzi au safari za usiku. Ni dalili inayoonyesha kuwa yameruhusiwa mambo kama hayo katika hali kama hizo, sio kuyafanya kuwa ni somo katika kulea na kufanya Da'wah, kama inavyofanya leo pindi wanafunzi wanapojifunza Anaashiyd hizi na kuziita kuwa ni "**Anaashiyd za Kiislamu**" au "**Anaashiyd za kidini**". Hii ni Bid'ah katika dini na zinatoka katika dini ya Suufiyyah iliyozushwa. Wao ndio wenye kujulikana kufanya Anaashiyd kuwa ni kipengele cha dini.

Ukikataza watu kuimba waambiwa kuwa ni mkali ni kwa nini unakataza nyimbo. Kwa nini unakataza pia picha watu waangalia TV[33] zao halafu wewe unawakataza. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anasema: **"Hakika Malaika hawaingii nyumba ambayo ina mbwa na picha"**[34]

Sasa tusiwakataze watu mapicha na Malaika hawaingii nyumbani mwao. Vipi tusiwakataze watu mapicha? Twaambiwa ni wakali tukiwakataza watu mapicha. Kuwakataza watu nyimbo ni ukali huo? Hadiyth zinakataza mambo haya kabisa. Amesema (Ta'ala):

﴿وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَشۡتَرِي لَهۡوَ ٱلۡحَدِيثِ لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ بِغَيۡرِ عِلۡمٖ وَيَتَّخِذَهَا هُزُوًاۚ﴾

**"Na katika watu wako wanaonunua maneno ya upuuzi ili wapoteze watu na njia ya Allaah bila elimu na wanaichukulia mzaha."** (31:06)

Abdullaah bin Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) anasema: "Ninaapa kwa yule ambaye hakuna mungu wa haki isipokuwa Yeye; ni nyimbo."[35]

---

= Ni wajibu kuzindua kampeni hizi na kupiga marufuku kuuzwa mikanda hii. Shari huanza ikiwa ndogo. Ikiwa mtu hazisimamishi mapema zitakuja kuendelea na kukua." (al-Khutwab al-Minbariyyah (03/184 185) Imaam Muhammad bin Swaalih bin Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) aliulizwa kuhusu Anaashiyd za Kiislamu kama inavyofuatia hapa chini:

**Swali**: Je, inajuzu kwa wanaume kuimba Anaashiyd za Kiislamu? Je, inajuzu kuwapigia dufu wanapoimba? Je, inajuzu kuimba Anaashiyd mbali na sikukuu na sherehe?

**Jibu**: Anaashiyd za Kiislamu ni Anaashiyd zilizozushwa. Zimeshabihiana na waliyozusha Suufiyyah. Kwa hivyo inatakiwa kwa mtu kujitenga nazo mbali kwa mawaidha katika Qur-aan na Sunnah. Isipokuwa tu labda katika vita ili ziweze kusaidia kuleta motisha na Jihaad katika njia ya Allaah (Ta'ala). Ni vizuri. Anaashiyd zikifuatanishiwa na dufu zinakuwa bado ziko mbali kabisa na usawa. (Fataawaa ash-Shaykh Muhammad bin Swaalih bin Uthaymiyn (01/134-135))

**33.** Tambua Allaah anirehemu mimi na wewe katika yale anayoyapenda na kuyaridhia ya kuwa kupiga picha ni katika madhambi makubwa. Kumethibiti Hadiyth nyingi zinazoharamisha picha za viumbe wenye roho kwa sampuli zake zote. Bi maana ni mamoja zikawa za kuchora kwa mkono, picha za kisasa za camera na nyenginezo zote za viumbe wenye roho. Katika hizo zote wanachuoni wamevua zile picha za dharurah ambazo mtu hana budi kuwa nazo katika mahitajio yake ya kimaisha. Mfano wa picha hizo zilizovuliwa na wanachuoni ni za kitambulisho, pasipoti, leseni ya kuendesha gari na mfano wa hizo. Mbali na hizi zengine zote ni haramu kutokana na kuenea kwa dalili zilizoharamisha picha za viumbe wenye roho. Hivyo wamche Allaah wale wapiga na wapigwa mapicha.

**34.** al-Bukhaariy (3225), Muslim (2104) na an-Nasaa 'iy (5347).

**35.** al-Adab al-Mufrad (786).

Allaah anakusudia nyimbo katika Aayah hii. Sasa ukikataza nyimbo waambiwa kwamba haifai ni ukali huo na wanakwambia umwache tu aimbe. Si ukali. Ndio Uislamu na ndio Da'wah ya haki. Si Da'wah ya al-Ikhwaan al- Muslimuun. Sisi sio al-Ikhwaan al-Muslimuun. Hapana. Da'wah yetu ni ya kukataza machafu; na kuamrisha mema na kukataza maovu. Haina maana kwamba tutatendea kazi kanuni inayosema:

**"Tushirikiane katika yale tunayoafikiana na tupeane udhuru kwa yale tunayotofautiana."**[36]

---

**36.** Hii ndio kanuni inayotumiwa na Ahl-ul-Bid'ah na Hizbiyyuun wengi ambao ni vifaranga vya al-Ikhwaan al-Muslimuun na Suruuriyyah. Ndio maana wao hawaoni neno kushirikiana na wakhalifu kama Shiyah, Suruuriyyah, Ibaadhiyyah, Hajaawirah, Quibiyyah na mapote mengine yote ya kipotevu kwa kutendea kazi kanuni hii yenye kupotosha. Bali si ajabu katika safu ya al-Ikhwaan al-Muslimuun ukakuta manaswara, mayahudi na wakomunisti. Shaykh Jamaal bin Furayhaan al-Haarithiy (Hafidhwahu Allaah) amesema alipokuwa akiraddi kanuni hii ya kipotevu:

"Mapote ya ki-Hizbiyyah ya kileo kama Jamaa'at ut Tabligh, al Ikhwaan al Muslimuun, Qutbiyyah, Suruuriyyah na Haddaadiyyah ni miongoni mwa mapote yaliyotuingilia. Walinganizi wa Salafiyyah ambao wanajinasibisha na mfumo wa Salaf us Swaalih na kufuata mapokezi ni wajibu kwao kupambana na mapote haya ya ki-Bid'ah yenye kwenda kinyume na yale aliyokuwa nayo Mtume (Swalla Allaahu alavlu wa sallam) na Maswahabah zake. Haitakikani kuwapa nafasi mifumo yao ikatanua, bali ni wajibu kuwabana na kukata harakati zao kwa kueneza elimu ya Kishari'ah kwa mujibu wa dalili ya Qur-aan na Sunnah na juu ya ufahamu wa Salaf-us-Swaalih. Watu wanatakiwa kufunzwa Tawhiyd ambayo mapote haya wanaipuuzia na kuwashughulisha watu na siasa na hamasa.

Baadhi ya watu wametilia umuhimu, kama wanavyodai wenyewe, kuwaokoa watu na maasi na kuwaingiza misikitini na wakati huo huo wanawaacha wabaki na I'tiqaad zao za kishirki pale wanapowaacha kutafuta baraka kutoka kwenye makaburi, kutufu kwayo na kuwataka uokozi wafu.

Wengine wametilia umuhimu, kama wanavyodai wenyewe, kuleta umoja na kusameheana katika mambo ya tofauti za 'Aqiydah. Kwa sababu wanaonelea kuwa waislamu wanatengana mambo ya "Aqiydah yakitunzwa. Ndio maana utawaona waabudu makaburi, Khawaarij, Mu'tazilah, Jahmiyyah na Shiyah wako yao. Mfumo wao unahusiana na kukusanya tu. Wanachotilia umuhimu tu ni kutaka kuwa na idadi kati kubwa wafuasi. Kanuni yao ni:

**"Tushirikiane sote kwa pamoja katika yale tunayokubaliana na kupeana udhuru katika yale tunayotofautiana."**

Sisi sio al-Ikhwaan al-Muslimuun kabisa. Da'wah yetu ni yenye kuamrisha mema na kukatazana maovu. Mtu atake asitake hii ndio ibaadah na ndio Da'wah ya haki.

Kwa hiyo katika matope wanayopakaziwa walinganizi Salafiyyuun ni kwamba ni wakali. Lakini si kweli kwamba ni ukali. Mkisoma Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alivyokuwa akitoa Khutbah alikuwa macho yake yanakuwa mekundu na sauti yake inakuwa ya juu na huzidi ghadhabu yake kama kwamba analiamrisha jeshi na kuliambia:

**"Adui atakujieni asubuhi au jioni!"** [37]

Hivi ndivyo alivyokuwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Sasa twaambiwa tukitoa Khutbah tuchekecheke kidogo na huku kuwaambia watu wasinyoe ndevu!!! Hivi mtu ni mkali watu wanyoa, je ukichekacheka watafanya nini? Si watakata videvu vyao sasa!! Ndugu zangu! Hii ni shubha inatiwa matope Da'wah ya as-Salafiyyah kwamba eti tunafukuza watu kwa sababu sisi ni wakali. Lakini si kweli kwamba ni ukali. Huku ni kuamrisha mema na kukataza maovu. Kwa hiyo hii inawauma. Wale wanyoa kidevu inawauma. Wale wanaoburuza makanzu wanaumia. Lakini si kwamba walinganizi ni wakali. Hapana. Hakuna mkali katika sisi.

---

= Ni juu ya Ahlus Sunnah wal-Athar, Salafiyyuun, kuzifichua hali za mapote haya yenye kwenda kinyume, kuurahadharisha Ummah nayo, kuraddi utata wao na kuyaponda kwa dalili za Kishari'ah. Kadhalika ni juu yao kulingania katika mfumo wa Salaf us-Swaalih (Radhiya Allaahu 'anhum) na kupanda 'Aqiydah ya Salafiyyah kwenye mioyo ya vizazi vinavyokuja huko mbeleni kama ambavyo wahenga wetu walipanda kwenye mioyo yetu." (al-Ajwibah al-Mufiydah 'an As-ilat il-Manaahij al Jadiydah, uk. 66-68)

**37.** Mwanachuoni Rabiy al-Madkhaliy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Anakuwa hivyo kutokana na khatari ya Bid'ah katika Ummah." (Sharh Usuw-il-Sunnah, uk. 367)

## 09. Shubha ya Sita: SALAFIYYUUN WANAWAPAKA MAFUTA VIONGOZI

Katika shubha ambazo zinapakaziwa Da'wah hii ni kwamba inawapaka mafuta viongozi. Wanasema kuwa Da'wah hii inawapaka mafuta viongozi na kuwapendelea. Hii pia ni shubha nyingine.

Da'wah hii inawajibisha kuwatii viongozi wa waislamu. Ni lazima waislamu wawatii viongozi wao. Isipokuwa maasi. Wakiamrisha maasi katika hali hiyo kutakuwa hakuna utiifu kwa wakiamrisha maasi. Lakini ni wajibu kuwatii viongozi kama hawakuamrisha kiumbe katika kumuasi Muumba. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) anasema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِي ٱلۡأَمۡرِ مِنكُمۡ﴾

**"Enyi mlioamini! Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wale wenye kutawalia mambo yenu." (04:59)**

Aayah inaamrisha kuwatii viongozi na kwamba kuwatii viongozi ni lazima. Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ni nyingi katika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy na "as-Swahiyh" ya Muslim. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anasema:

**"Mwenye kunitii mimi ndio amemtii Allaah na mwenye kuniasi mimi ndio amemuasi Allaah. Mwenye kumtii kiongozi amenitii mimi na mwenye kumuasi kiongozi ameniasi mimi."** [38]

Hadiyth ziko wazi katika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy na Muslim. Hii ndio 'Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah. Bali suala hili limewekwa katika vitabu vya 'Aqiydah[39] Suala la kuwatii viongozi limewekwa katika vitabu vya 'Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah ili kuonesha umuhimu wake.

---

**38.** Al-Bukhaariy (7137) na Muslim (1835).

**39.** Miongoni mwa vitabu vizuri vinavyobainisha 'Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa ah -kukiwemo suala hili- ni vifuatavyo:

1-"Usuwl-us-Sunnah" cha Ahmad bin Hanbal.

2-"al-'Aqiydah al-Waasitwiyyah" cha Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah.

3-"Lum'at-ul-I'tiqaad" cha Ibn Ibn Qudaamah.

4-"al-'Aqiydah at Twahaawiyyah" cha at-Twahaawiy.

5-"Sharh-us-Sunnah" ya Barbahaariy.

6-"ash-Shari'ah" cha al Aainin.

Leo wanakuja watu wanasema kuwa Da'wah Salafiyyah inawapaka mafuta viongozi. Sasa dalili hizi tuzifanye nini? Tuache dalili hizi za Qur-aan na Sunnah kwa ajili ya maneno yao? Hapana. Ni lazima zitekelezwe dalili hizi. Ni lazima tuwatii viongozi katika yasiyokuwa maasi. Amesema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

**"Ni juu ya kila muislamu kumsikiliza na kumtii kiongozi katika analopenda na analolichukia. Ni lazima amtii kiongozi wake."**[40]

Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ziko wazi. Halafu leo wanasema Da'wah Salafiyyah inawapaka mafuta viongozi na kwamba inawapendelea viongozi. Uhakika wa mambo ni kuwa Da'wah Salafiyyah haina haja ya uongozi. Si kwamba kuna walinganizi wa Salafiyyuun ambao wanapigania mtu awe raisi.[41] Hapana. Lakini ni lazima tuangalia haki ni nini Quran na Hadiyth inachosema. Ni lazima tuzifuate.

Kwa hiyo suala hili la kuwatii viongozi ni suala la lazima kwa waislamu. Lazima wawatii viongozi wao katika isiyokuwa maasi. Kama wakiamrisha maasi katika hali hiyo hawatiiwi viongozi. Lakini vinginevyo tunawajibika kuwatii viongozi kulingana na Aayah za Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) na Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

---

7-"Sharh Usuwl-il-I'tiqaad Ahl-is-Sunnah" cha al-Laalakaa'iy.

8- "as-Sunnah" cha al-Khallaal.

9-"as-Sunnah" ya Ibn Haatim.

10-as-Sunnah" ya at-Twabariy.

11-"al-Ibaanah" ya Ibn Battwah.

12-"Aqiydah-us-Salaf wa Asw-haab-il-Hadiyth" cha as-Swaabuuniy.

13-"at-Tawhiyd" cha Ibn Khuzaymah. Vipo vyengine vingi tu.

**40.** al-Bukhaariy (7144), Muslim (1839), Abu Daawuud (2626) na an-Nasaa iy (4206).

**41.** Hii ni kazi ya al-Ikhwaan al-Muslimuun ambapo wanafanya kila bidii na kutumia kila njia iwezekanayo hata kama itakuwa ni kwa kuwafanyia uasi watawala wa Kiislamu, mauaji ya kuvizia, mapinduzi na mambo mengine ya haramu - ili kufikia malengo ya muanzilishi wa kundi hili ambaye si mwengine ni Hasan al- Bannaa (aliyefariki. 1347). "Allaamah Zayd bin Muhammad al-Madkhaliy (Rahimahu Allaah) amesema alipokuwa akikosoa mfumo wa kundi hili ifuatavyo:

Imaam at-Twahaawiy ameelezea:

"Hatuoni sisi kutoka katika utiifu wa kiongozi wetu hata kama wakiwa ni madhalimu."

Hivi ndivyo anavyosema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): **"Msikilize na umtii kiongozi hata ukipigwa mgongo wako na ikachukuliwa mali yako."**[42]
Hapa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anamwambia Mu'aadh (Radhiya Allaahu 'anh).

Kwa hiyo kumtii kiongozi ni katika wajibu wa kila muislamu. Haina maana ni kuwapaka mafuta viongozi. Hapana! Ni amri ya Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) na ni amri ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Kuwaasi viongozi ni maasi. Bali ni katika Ujaahiliyyah. Shaykh Muhammad bin 'Abdil- Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema katika "al-Masaa-il al-Jaahiyyah" ambayo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliwakhalifu kwayo washirina. Moja wapo aliweka suala hili kwamba ni katika masuala Jaahiyyah. Wao walikuwa wakiona kuwaasi viongozi ndio utukufu na kuwatii ni udhalilifu. Hawa ni watu wa ki-Jaahiliyyah. Lakini waislamu sivyo. Waislamu kuwatii viongozi ni amri ya Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) na ni amri ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na wala si udhalilifu. Bali ni jambo lina maslahi.

Hizi ni baadhi ya Shubha nyingi ambazo inapakaziwa Da'wah Salafiyyah.

Haya ni madogo tu katika mambo mengi. Yote ni ya batili. Hakuna hata moja la haki wanalolipakazia Da'wah Salafiyyah. Yote ni batili.

---

= "Wanajibidisha kufikia uongozi. Wanatumia fursa kwa nembo zao ili kwa njia zote waweze kuhudumia mfumo wao. Kwa ajili hiyo utawaona namna ambavyo wanapambana tu na watawala ambao wao wanaonelea kuwa ni washirikina katika Haakimiyyah. Hawajali shirki inayofanywa katika ibaadah ambayo Mitume wote ndio walianza kupambana nayo na kuwalingania watu kujiepusha nayo." (Asbaab Istiqaamat ish-Shabaab wa Bawaa 'ith Inhiraafihim, uk. 24).

**42.** (Fath-ul-Baariy (08/13))

Kwa hiyo ndugu zangu waislamu! Da'wah Salafiyyah ndio Da'wah ya haki. Ama Da'wah zingine zote ni za batili na hazina dalili yoyote katika Qur-aan wala Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Kwa hiyo waislamu sote tunawajibika kufuata mfumo huu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake na kufuata 'Aqiydah ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake. Tusipofuata tutapotea

Hii ni kwa Aayah ya Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala):

﴿وَمَن يُشَاقِقِ ٱلرَّسُولَ مِنۢ بَعۡدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ ٱلۡهُدَىٰ وَيَتَّبِعۡ غَيۡرَ سَبِيلِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ نُوَلِّهِۦ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصۡلِهِۦ جَهَنَّمَۖ وَسَآءَتۡ مَصِيرًا﴾

**"Na atakayempinga Mtume baada ya kumbainikia uongofu na akaifuata njia isiyokuwa ya waumini, Tutamgeuza alikogeukia na tutamuingiza Motoni - na motoni ni mbaya marejeo yake!" (04:115)**

Kwa hiyo ndugu zangu waislamu! Msipofuata mfumo huu wa Mtume na Maswahabah wake, mjue mtapotea.

Tunamuomba Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kwa majina Yake mazuri na sifa Zake kuu Atujaalie miongoni mwa wale wenye kusikia maneno na kufuata yaliyo mazuri. Utakasifu na himdi zote ni Zako Allaah. Ninashuhudia ya kwamba hapana Mola mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye. Ninakuomba msamaha na kutubia kwako.

Ninamuomba Allah atawafikishe sote kwa elimu yenye manufaa na amali njema.

**وبالله التوفيق**

2/6/1437